# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI
# TEMEKE MASASI SECONDARY SCHOOL

**EDUCATION FOR SELF EMPLOYMENT"**
**IS OUR MOTTO**

Mkuu wa Shule: 0719807040
Makamu Mkuu wa Shule : 0763378530
Mtaaluma 0778417641
Tarehe ……………

Temeke Masasi Sekondari School
P. O box 447,
Masasi.

**Jina la Mwanafunzi**………………………………………...……….

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI TEMEKE MASASI HALMASHAURI YA MJI MASASI. MKOA MTWARA MWAKA……….**

**1.0:** Kwa niaba ya kamati ya uchaguzi ninayo furaha kukuarifu rasmi kwamba umechaguliwa kujiunga na shule hii kidato cha **tano** Tahasusi ya...............mwaka…….. **EDUCATION FOR SELF EMPLOYMENT**" maneno hayo ndiyo **KAULI MOTTO** au mwongozo wa shule yetu. Ukiwa umekubali kujiunga na shule hii basi huna budi kuitafakari kauli hiyo.

Shule ya Sekondari Temeke Masasi ipo umbali wa kilometa Saba Magharibi mwa mji wa Masasi. Usafiri kutoka mjini Masasi kuja shuleni unapatikana katika kituo kikuu cha mabasi/stend kuu. Nauli ni shs. 4000/= kwa pikipiki na 5,000 kwa Bajaji. Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe
Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe **………………** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **…………..**

**2.0: Mambo muhimu ya kuzingatia**

**2.1: Sare ya shule**

(a) Sare za darasani ni:

- Sketi Mbili Rangi ya chungwa (Orange) -Rinda Box, Isteem namba moja ni nzuri zaidi. Picha ya mshono imeambatanishwa, ni lazima sketi iwe ndefu kama inavyoonekana kwenye picha ya mshono.
- Shati nyeupe mikono mirefu na isiyobana **[WAKRISTO].** Nusu kanzu na hijab[**Kijuba**] nyeupe isiyofunika goti, mikono mirefu **[WAISLAM]** jozi mbili.
- Raba nyeupe za kufunga na kamba zenye kisigino kifupi jozi mbili
- Soksi nyeupe zisizo na urembo au alama zozote za rangi angalau jozi mbili.
- Sweta rangi ya **Blue (Bluu)** mikono mirefu isiyo ya kola.

(b) Sare za kushindia **[Shamba dress]** ni gauni yenye mikono mifupi mtindo wa solo rangi ya **Dark blue** mbili. Picha ya mshono [**imeambatanishwa**]. (Kitambaa cha Isteem namba 1 ni kizuri zaidi). Ni vema hijabu kwa Waislam iwe nyepesi na ifanane na sare ya kushindia [**shamba dress**]

(c) Sare za michezo ni T-shirt rangi ya light grey **[Kijivu nyeupe]** yenye kola-02, Truck suit nyeusi isiyobana mwili yenye mchirizi mweupe pembeni na raba nyeusi. T-shirt Zinapatikana shuleni.

(d) Tai ndefu mbili isivuke kitovu **[rangi ya Orange]** ifanane na rangi ya sketi ya shule **[kwa Wakristo]**

**Muhimu**:

**Nguo za nyumbani haziruhusiwi kabisa shuleni. Aidha mwanafunzi anaposafiri kuja shuleni avae sare ya shule.**

**2.2 Michango mbalimbali**

| Na | Aina ya mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5,000/= |
| 3 | Nembo | 5,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 4 | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| 5 | **Jumla** | **80,000/=** |

**MUHIMU:**

- Ulipaji wa michango yote ufanyike kwa njia ya Benki () Jina la akaunti ni **TEMEKE MASASI SECONDARY SCHOOL.**
- **Michango** ilipwe kwenye **.**
- Usisahau kuandika jina kamili laMwanafunzi .Risiti (paying slip) iletwe kwa Mhasibu siku ya kufungua shule, **(mara tu mwanafunzi anaporipoti shuleni).**
- Malipo yanayofanyika kwa wakala toa nakala ya **Risiti.**
- **BIMA YA AFYA :- - mwanafunzi mwenye Bima ya afya aje nayo shuleni**

**= Mwanafunzi asiye na Bima ya afya, anachangia Bima ya NHIF yenye gharama ya Tsh. 50,400/= kwa Mwaka Mmoja.**

**2.3: Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni**

i)Madaftari 10 caunter book, kalam na mkebe wa hesabu
ii)Shuka mbili rangi nyeupe,blanket 1,foronya 1,chandarua 1 nyeupe
iii)Nguo za ndani za kutosha (chupi, shimizi, sidiria, Tight fupi rangi nyeusi au nyeupe)
iv)Ream ya karatasi, 2 (Size A4) kwa mwaka.
v)Scientific calculator kwa wanafunzi wa sayansi na Jiografia .
vi) Godoro la futi mbili na nusu kwa ftr 4.
vii)Mafuta ya kupaka yasiyo na viambata vya sumu **[cream]** na harufu kali.
viii)Kanga au kitenge (jozi moja tu)
ix)Chandarua rangi nyeupe, Taulo, Mswaki, Dawa ya meno, Sabuni yakufulia na kuogea.
x) Nakala ya hati ya **Matokeo kidato cha iv au" Result slip".**
xi)Nakala ya **cheti cha kuzaliwa.**
xii)Picha ya mwanafunzi 1, ya wazazi /walezi mojamoja, na ndugu wa karibu wamwanafunzi picha moja
xiii).Vyombo vya chakula[Sahani,Bakuli,Kijiko na Kikombe]
xiv).Ndoo mbili ndogo zenye mfunikona kikopo cha kuogea

**2.4: VIFAA VYA USAFI AMBAVYO MWANAFUNZI ANATAKIWA AJE NAVYO**:

(a) Wanafunzi wote wanatakiwa kuja na taa inayotumia solar au betri ya kutumia pale inapotokea dharula ya kukatika kwa Umeme. Taa hiyo isiwe na mifumo ya kuchaji kwenye umeme (isitumie usb kuchajia).

(b) Vifaa vifuatavyo viletwe kulingana na TAHASUSI kama ilivyo katika jedwali,

| **TAHASUSI** | **VIFAA** |
|---|---|
| HGK | Dawa ya chooni ya maji lita 5, fagio ya kawaida ya wima ya kufagilia nje, jembe lenye mpini, hard broom ya kusafishia choo na bafu. |
| HGL | Dawa ya chooni ya maji lita 5, fagio ya kawaida ya wima ya kufagilia nje, soft broom ya kufangilia ndani, fagio ngumu (hard broom) ya kusafishia choo na bafu,mopa (ya kukaushia maji),squizer (ya kusukumia maji). |
| HKL | Dawa ya chooni ya maji lita 5, fagio ya kawaida ya wima ya kufagilia nje, fyekeo, soft broom ya kufagilia ndani na squizer (ya kusukumia maji) |
| HGE | Dawa ya chooni ya maji lita 5, Fagio ya kawaida ya wima ya kufagilia nje,Soft broom ya kufagilia ndani, Fagio ngumu(hard broom) ya kusafishia choo na bafu, Mopa(ya kukaushia maji), Squizer(ya kusukumia maji). |

**3.0: SHERIA NA KANUNI ZA SHULE**

i. Heshima kwa viongozi, Wazazi, Wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku na alfajiri (Morning and Night Preparation).
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa.
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndan na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya Shule.
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
ix. Kutunza mali za Shule.
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari: na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU**;

- ❖ Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yeyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi
- ❖ Mwanafunzi haruhusiwi kuja na chakula cha aina yoyote shuleni.
- ❖ Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu.
- ❖ Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalumu toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa)
- ❖ Mwanafunzi haruhusiwi kuja na flash,laini ya simu,memory card,redio, usb,chaja ya simu, adapta,earphone, smart watch na vitu vingine mfano wa hivyo.

**4.0: MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.**

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/ Utoro
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, waalimu/ walezi na jamii kwa ujumla.
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule
vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya
viii. Uvutaji wa sigara
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu

Uharibifu wa mali za umma kwa makusudi.
Fomu hii ya kujiunga na shule inatakiwa irudishwe ofisini pamoja na cheti cha kupima kilichojazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali ambacho pia kimeambatanishwa. Hakikisha umetoa nakala ya fomu hii kwa ajili ya rejea yako.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

Jina la Mkuu wa Shule……………….

**MKUU WA SHULE**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (Wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na**

**watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa watoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/ MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO:-**

- **MKUU WA SHULE: 0719807040**
- **MAKAMU MKUU WA SHULE: 0763378530 AU**
- **MWANDAMIZI TAALUMA: 0778417641**
- **MWANDAMIZI NIDHAMU: 0653475025**

**TEMEKE MASASI SECONDARY SCHOOL,**

**P.O. Box 447,**
**MASASI**

**Ref. No. ………………………………..** **Date ……………………………..**

**PART A:**
**To the Medical Officer,**
**…………………………………………….**
**…………………………………………….**
**…………………………………………….**

**REF:** ……………………………………………………………………………….
Please examine the above named student as to her physical and mental fitness for being student. Each defect will hinder a girl for Secondary School Education.

1. (a) Eye sight
   (b) Hearing
   (c) Limbs
   (d) Speech
   (e) Venereal Disease
   (f) Leprosy
   (g) Epilepsy
2. Neurosis
3. Other serious diseases
4. Pregnancy

**PART B: MEDICAL CERTIFICATE**
(To be completed by a GOVERNMENT MEDICAL OFFICER):
I have examined the above named student and consider that she is physically fit/not fit for a full time Secondary School Education.

(a) Eye sight ……………………………… (f) Leprosy ……..................................
(b) Hearing ………………………………. (g) Epilepsy ………………………….
(c) Limbs…………………………………. (h) Neurosis ………………………….
(d) Speech ………………………………… (i) Other serious disease ……………..
(e) Venereal diseases ……………………. (j) Pregnancy …………………………

**Date…………………………..** **Signature………………………………**

**Station ………………………** **Designation ………………………….**

# MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. Jina la Kamili…………………………………………………………………………
(kama lilivyo kwenye self form)
2. Tarehe ya kuzaliwa……………………………………………………………......
3. Anwani ya nyumbani………………………………………………………………
4. Mahali unapoishi(nyumbani kwenu) : Wilaya…………......Tarafa……………….
Kata………………………….Kijiji……………………………………………….
5. Shule ya sekodari uliyotoka………………………………………………………
6. Dini……………………………………………………………………………...
7. Kabila…………………………………………………………………………...
8. Taifa(Mtanzania/Si Mtanzania)…………………………………………………...

**9. Jamaa katika familia(Watakaohusishwa katika malezi ya mwanafunzi akiwa hapa shuleni)**

(i)Jina la Baba…………………………………………………………...
Anuani………………………………Namba ya simu……………………..
Anaishi/Haishi………………………………………………………...
Kazi yake……………………………………………………………...

(ii) Jina la Mama……………………………………………………………….
Anuani………………………………Namba ya simu……………………..
Anaishi/Haishi………………………………………………………...
Kazi yake……………………………………………………………...

(iii) Jina la Mlezi/Ndugu……………………………………………………….
Anuani………………………………Namba ya simu……………………..
Anaishi/Haishi………………………………………………………...
Kazi yake……………………………………………………………...

**10. Mkataba wa Mwanafunzi kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai**

Mimi…....................................... (Mwanafunzi) nakiri kuwa, nimezisoma sheria, kanuni na taratibu za shule kwa umakini na utulivu mkubwa. Hivyo basi ninaahidi: "Nitazifuata Sheria, Kanuni na Taratibu za shule kama zilivyoelekezwa Aidha ninaamini kuwa Sheria na Taratibu zipo kwa nia ya kunisaidia katika Nyanja zote muhimu ikiwa ni pamoja na nidhamu, maadili na taaluma." Vilevile naahidi kuwa sitoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai. Kinyume na hivyo hatua stahiki za kinidhamu zichukuliwe dhidi yangu.

**……………………………..**      **……..……...…………**


**Sahihi ya mwanafunzi**      **Tarehe**

**11. Form ya Mzazi/Mlezi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo yaliyotolewa na shule**


Mimi……………………………(Mzazi/Mlezi) wa Mwanafunzi… ......................... Ninakiri kuwa, nakubaliana na sheria, kanumi na maelekezo yote yaliyotolewa na shule. Hivyo basi niko tayari mtoto wangu asome katika shule hii nitakuwa tayari kumpa kila aina ya msaada utakaohitajika katika kufanikisha masomo yake na malezi yake kwa ujumla akiwa hapa shuleni kwa kipindi cha miaka miwili (2).

| | |
|---|---|
| **……………………………..** | **……...…………………** |
| **Sahihi ya Mzazi/Mlezi** | **Tarehe** |

SARE ZA SHULE



SARE ZA SHULE



SARE YA KAZI




SARE YA KAZI
ZIP
GAUNI